THE TIMER NATIONAL SERIES
JUNIOR SCHOOL ASSESSMENTS 2024
SHUGHULI ZA KISWAHILI {8}

JS 0032024

JINA LA MTAHINIWA: .....

NAMBARI YA UTAHINI: .....

JINA LA SHULE: ..... TAREHE: .....

ZOEZI 1 : KUSOMA

KUSOMA KWA UFAHAMU

Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali.

Katika nchi ya Ustawi, wananchi wengi walipata ari ya kujiandalia maisha bora ya baadaye. Walithamini sana mustakabali wa wana wao. Ili kufanikisha haya, waliunda vyama vya ushirika. Wananchi walipata mikopo isiyo na riba kubwa. Wananchi wa Ustawi walipambana kwa hali na mali kuimarisha hali yao ya maisha. Muda si muda, vyama vikastawi. **Fedha walizopata zilivunja nguu na milima ikalala**. Kwa wananchi wengi wa Ustawi, biwi la mashaka tipitipi liliondolewa na baadaye wakaanza kuishi kama watu. Usimamizi mzuri wa vyama ulizaa matunda yaliyowafaa wananchi wote.

Baada ya uchaguzi wa wanachama, uongozi mpya ulishika hatamu. Lakini kumbe ngoma ya wana haikeshi! Viongozi waliojawa na tamaa walivuruga usimamizi wa vyama. Ahadi za kuendeleza na kuboresha vyama vya ushirika zilitupwa katika jaa! Walitumia hila kujipa mikopo mikubwa ambayo hawakulipa. Matumizi yasiyo na mipango yaliwekwa katika ratiba. Wengine walipora mali ya wanachama. Kutokana na wizi na wanachama kuchezeshwa ngoma, vyama vilianza kulegalega. Ukweli wa wakubwa kuwameza wadogo ulianza kubainika. Wanachama walijuta kwa kutojua kuwa paka hawekewi maziwa kuiinda.

Wananchi waliingiwa na kiwewe. Waliogopa kurudia umaskini wa hapo awali. Waliililia serikali, nacho kilio chao kikasikika. Serikali iliagiza vyama vyote visajiliwe na kuunda katiba. Sheria aidha iliweka vigezo vya watu wanaopaswa kuongoza vyama. Miongoni mwa vigezo hivyo vilikuwa ni elimu, tajriba, maadili na uwajibikaji. Kwa amri ya serikali, madaftari ya uhasibu wa vyama yalikaguliwa. Waliopatikana na hatia **walikula kalenda**. Bunge la nchi lilitunga sheria nzuri zilizolenga kulinda vyama vya ushirika. Mapato ya vyama yakaanza kuimarika.

1. Kuundwa kwa vyama vya ushirika kulikuwa na umuhimu gani kwa wananchi wa Ustawi? **(alama 1)**

_____

_____

2. Eleza maana ya kidokezi kilichoangaziwa katika paragrafu ya kwanza. **(alama 2)**

_____

_____

_____

3. Ni nini hasa kilichowaondolea wananchi wa Ustawi mashaka yaliyowazonga? **(alama 1)**

_____

_____

4. Uongozi mpya uliwaletea wanachama wa vyama vya ushirika maafa gani? **(alama 1)**

_____

_____